HOTUBA YA MHE. JOHN V.K. MONGELLA, MKUU WA MKOA WA MWANZA WAKATI WA KUADHIMISHA MIAKA ISHIRINI NA MOJA (21) YA AJALI YA MELI YA M.V. BUKOBA TAREHE 21/05/2017

Mhe. Mary Tesha Onesmo, Mkuu wa Wilaya Nyamagana,
Mhe. Dkt Leonard Masale, Mkuu wa Wilaya Ilemela,
Ndugu. Eric Hamissi, Kaimu Meneja Mkuu Kampuni ya Huduma za Meli – MSCL,
Wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama Mkoa,
Wahe. Viongozi wa dini,
Ndugu Wanafamilia,
Wageni wote,
Mabibi na Mabwana.
Itifaki imezingatiwa.

Awali ya yote, nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, kwa kutulinda na kutuwezesha kukutana hapa leo. Vilevile kwa niaba ya wakazi wa Mkoa wa Mwanza, napenda nianze kwa kuwashukuru sana nyote kwa kutenga muda wenu ili tushirikiane kwa pamoja katika kuwakumbuka na kuwaombea ndugu zetu Wahanga wa ajali ya Meli ya M.V. Bukoba iliyotokea tarehe 21/5/1996. Aidha, siku hii ni muhimu kwetu kwa ajili ya kufanya tathmini ya mafanikio na changamoto zilizopo katika kukabiliana na hali ya usalama majini.

Shukurani nyingi pia ziwaendee Kampuni ya Huduma za Meli – MSCL, ambao ni waandaaji wa kumbukumbu hii muhimu kwa kazi kubwa waliyoifanya.
Aidha, naomba niwashukuru wale wote ambao walishirikiana nasi katika kukabiliana na hali ngumu ya uokozi na uopoaji wa miili ya wapendwa wetu wakati ajali hii mbaya ilipotokea.

Ndugu wanafamilia na wageni wote, leo tumekusanyika hapa kwa ajili ya kumbukumbu ya miaka ishirini na moja (21) ya ajali mbaya ya Meli ya M.V. Bukoba ambayo iliteketeza mamia ya wapendwa wetu. Ni jambo la kuhudhunisha sana, lakini **Mtume Paulo** anatufariji kwa yale aliyoyasema kwa Wathesolonike kwamba."Furahini siku zote, ombeni bila kukoma, shukuruni kwa kila jambo; maana hayo ni mapenzi ya Mungu kwenu katika Kristu Yesu". (1 Wathelonike 5:16-18).

Ndugu zangu, Ni kweli kifo hakizuiliki. Kinaleta simanzi kubwa hasa tunapoondokewa na wale tuwapendao. Tujipe moyo na nguvu kwamba hili lilitokea na hatuna budi kulikabili.

Ndugu zangu, kufuatia ajali hiyo mbaya katika historia ya Nchi yetu, Serikali imechukua na inaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kudhibiti majanga ya namna hiyo,

japo pamoja na hatua hizo bado ajali za majini za hapa na pale zinatokea.

Naamini sana kuwa tuna kila sababu ya kuendelea kutafuta suluhisho la kudumu kwa kutekeleza mikakati yetu mbalimbali kwa uendelevu bila kuacha mwanya kadri itakavyowezekana.

Ndugu zangu, hatua kadhaa zimechukuliwa ikiwa ni pamoja na: -

1. Yamefanyika marekebisho ya sheria “Amendment of the Merchant Shipping Act 1967 – To Merchant Shipping Act 2003” ambayo ni sheria mama ya usafiri wa majini.

2. SUMATRA imeanzisha kituo maalum cha kuratibu, kufanya utafutaji na uokoaji majini (kwenye ziwa Victoria). Kituo hiki ambacho kipo Jijini Mwanza kimeanzishwa mwaka 2017, Pia, kinatoa taarifa za hali ya hewa kwenye Ziwa Viktoria.

3. Tanzania imeridhia baadhi ya sheria za Kimataifa zinazosimamiwa na Shirika la usafiri majini Duniani (**IMO - International Maritime Organization).**

Sheria hizo zinazingatia:

I. Uwepo wa **vifaa vya usalama** (SOLAS - Safety of Life at Sea).
II. Ukubwa na uwezo wa meli kubeba (loading) mizigo na abiria
III. Ubora wa mafunzo wa Mabaharia (Standard of training and Certification).

4. Tanzania imekwisha ingizwa kwenye orodha (white list) ya (IMO- International Maritime Organization). Aidha, Chuo cha Mabaharia cha Dar es Salaam (DMI) kimekuwa ndicho Chuo kinachotambulika kwa mafunzo ya Mabaharia kwa nchi za Africa Mashariki na Kati.

5. SUMATRA inao Maafisa wakaguzi hapa ziwa Victoria katika Makao Makuu ya Mikoa ya Mwanza, Bukoba, na Kagera. Aidha, Wilaya ya Ukerewe imepewa nafasi ya pekee kwa kuwa na wakaguzi wa SUMATRA kwenye Wilaya hiyo.

Ndugu wananchi, vile vile SUMATRA imekuwa ikitoa hati ya usafiri ambapo pia kumekuwepo na mfumo wa ukaguzi wa kila mwaka unaotolewa cheti cha majaribio ya usalama wa vyombo vya majini. Aidha, kiwango cha Mabaharia katika chombo na sehemu yao kinatazamwa pia wakati wa ukaguzi wa vyombo.

Ndugu zangu, wananchi kwa ujumla, napenda kuchukua fursa hii pia kutoa wito kwa wasafirishaji na wasafiri kuzingatia usalama ili kukabiliana na ajali zinazoweza kuzuilika.

Nawaombeni sana ndugu zangu mnaotumia usafiri wa majini, kusaidia kutoa taarifa katika vyombo husika pale mnapoona kuna dalili za uzembe wa kutozingatia usalama ili hatua zichukuliwa mapema kabla ya ajali kutokea. Aidha, nawaombeni sana msikubali kupanda vyombo vya usafiri vilivyojaa kupita kiasi na vile vyombo visivyo imara.

Vilevile, nawaombeni wananchi wote kushirikiana na Serikali katika kuhifadhi kumbukumbu hizi muhimu kwa ajili ya ndugu waliotutoka. Nimeambiwa kuna watu wanayatumia vibaya maeneo ya kumbukumbu hizi, wapo waliofanya maeneo haya vijiwe vya kuvutia bangi. Nachukua fursa hii kuwaonya waache mara moja, na wananchi watusaidie kuwafichua ili hatua kali dhidi yao zichukuliwe.

Natoa wito kwa SUMATRA, kuendelea na majukumu yake ipasavyo, ikiwa ni pamoja na:

- Kufuatilia na kupata taarifa za hali halisi ya usafiri wa Nchi kavu na Majini.

- Kushughulikia kero mbalimbali zinazohusu usafiri wa barabara na majini zikiwemo za mabasi ya mikoani na daladala.
- Kushiriki kikamilifu katika kufuatilia hali ya Usafiri wa nchi kavu na majini
- Kujitangaza katika vyombo mbalimbali vya habari ili majukumu yenu yaweze kufahamika kwa wananchi wote.

Ndugu wanafamilia, wageni wote,
Mabibi na Mabwana,

Naomba nimalize kwa kutoa tena pole kwa ndugu, jamaa na marafiki wote wa marehemu. Napenda kuchukua nafasi hii kuwaombeni nyote kila mmoja kwa imani yake kuwaombea ndugu zetu hawa waliotutangulia mbele za haki ili Mwenyezi Mungu azilaze roho zao mahali pema peponi. **A m i n a!**